# OFISI YA WAZIRI MKUU

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI

MKOA WA ARUSHA
Barua zote ziandikwe kwa Mkuu wa Shule

**Simu Na. +255752954965**

IRKISONGO SEKONDARI,
S.L.P. 43,
MONDULI.

Kumb. Na. H/W/MOND/SS/IRK/2026 …………………………..

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA IRKISONGO HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI, MKOA WA ARUSHA.**

**Ndugu mzazi/mlezi,** Uongozi wa Shule ya Sekondari Irkisongo unayo furaha kukuarifu kuwa mwanao ……………………………............................................................................................................... amechaguliwa kujiunga na kidato cha 5 katika Shule ya Sekondari Irkisongo mwaka, …………. Shule ya Sekondari Irkisongo ipo umbali wa kilometa 45 kutoka Arusha mjini na usafiri wa kutoka Arusha mjini unapatikana kituo cha mabasi ya stendi ndogo kwa nauli ya sh. 3,000/= hadi Monduli mjini.

Shule ipo Monduli mjini Kaskazini mwa kituo cha mabasi Monduli hatua 300 kutoka kituoni. Shule yetu ni ya wasichana tu kidato cha kwanza hadi cha sita.

Shule itafunguliwa tarehe ....................... hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe hiyo na si vinginevyo.

## SARE ZA SHULE

I. Sketi mbili rangi ya blue bahari (light blue) mshono"rinda box" ndefu mpaka kwenye kisigino.
II. Shati mbili nyeupe Tetron mikono mirefu isiyobana mwili.
III. Viatu vyeusi jozi mbili vya ngozi na sio vya ghorofa, vya kufunga kamba.
IV. Sweta bluu bahari (light blue) ya V shingoni na michirizi mieupe shingoni na mikononi)
V. Aje na Soksi ndefu nyeupe zinazofika kwenye magoti jozi mbili
VI. Tai rangi ya blue bahari yenye miraba mieupe.
VII. Picha 2 za passpoti (PPS) ya Baba na Mama au Mlezi.

## SARE ZA KUVALIWA BAADA YA MASOMO

I. Gauni rangi ya blue bahari yenye mshono wa solo ndefu mpaka kwenye kisigino.
II. Track suit ya kuvaliwa usiku rangi ya blue bahari (light blue) yenye mistari mieupe pembeni isiyobana mwili.

III. T – Shirt ya rangi ya blue bahari yenye kola isiyo na maandishi wala picha yoyote
IV. Raba za kufunga kwa kamba kwa ajili ya michezo
V. Mabuti ya kuvaa wakati wa mvua na Mwamvuli mmoja

**VIFAA VYA DARASANI**

- Madaftari makubwa 13 "COUNTER BOOK"QUIRE 3
- Madaftari madogo 7
- Mkebe "Mathematical Set"
- Kamusi ya Kiingereza (Oxford/Longman Dictionary)
- Kalamu za kutosha, rula na penseli

**VITABU**

Kila mwanafunzi aje na vitabu vya mchepuo wake kwa kila somo kama ifuatavyo:-

**1. ECONOMICS**

i. Simplified Economics by N. A. Saleemi
ii. Modern Economics by Robert Mudida
iii. Economics 1 & 2 by Ambilikile
iv. Economics by chand

**2. ADVANCED MATHEMATICS;**

(i) Pure Mathematics 2 by J. K Backhouses
(ii) Pure mathematics 1 by C.J Tranter
(iii) Advanced mathematics book five (5) by Silem I. Septine
(iv) Advanced mathematics book six (6) by Silem I. Septine
(v) S. Chand mathematics class XI volume I
(vi) S. Chand mathematics class XII volume II
(vii) Mayombi ,Advanced Mathematics Form Five
(viii) Advanced Mathematics Form Five by TIE

**3. GEOGRAPHY;**

(i) Advanced level Practical Geography by Zist Kamili
(ii) Human and Economic Geography by Msabila D. T.
(iii)Physical Geography by Msabila D.T
(iv)Physical Geography Advance S.S (TIE)
(v)Practical Geography for Advanced Sec.schools (TIE) 2025
(vi)Physical Geography New syllabus 2025 (By Zisti Kamili)

**4. ENGLISH:**

(i) English Language for Advanced Form Five by TIE
(ii) Competence in Linguistics by E. Mgonja.

5. **KISWAHILI :**
   (i) Dunia Uwanja wa Fujo (Euphrase Kezilahabi)
   (ii) Ua la Faraja by W.E.Mkufya
   (iii) Mirathi ya Hatari by C.G.Mung'ong'o
   (iv)Wasifu wa Binti Saad by Shaban Robert

6. **HISTORY:**
   (i) Basic Fact about the World History New syllabus 2025 by Shibitali Tumaini Ck (ii) The Ultimate Principe of History one by Magoti B

7. **HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI:**
   Historia ya Tanzania na maadili kidato cha Tano na Sita
8. **ACADEMIC COMMUNICATION:**
   Academic communication for advanced secondary schools, student book Form 5 & 6

**9. FASIHI YA KISWAHILI**

***TAHAKIKI YA KISWAHILI;***

**RIWAYA**;-

Vuta N' Kuvute (Shfi Adam Shafi)
Asali Chungu (Said Ahmed Mohamad)
Mwana wa Yungi Hulewa (Said Ahmed Mohamed)
Vipuli vya Figo (Emmanuel Mbogo)

**TAMTHILIYA;** -
Kaptula la Marx (Euphrase Kezilahabi)
Nyerere na Safari ya Kaanani (Emmanuel Mobogo)
Morani (Emmanuel Mobogo)

**USHAIRI; -**
Dhifa (Euphrase Kezilahabi)
Utenzi Mjumui wa Karne wa 21 (Idd M. Mwimbe)
Malenga wa Bara (M.M. Mulokozi na K.K. Kahigi)
Fungate ya Uhuru (Mohamed Seif Khatib)

**NADHARIA NA FASIHI –** MOGIRE DIANAH

**9. LITERATURE IN ENGLISH;**

***List of readings in Plays;***

- Betrayal in the City – **Francis Imbuga**
- I will marry when I want – **Ngugi wa Thiong'o & Ngugi wa Mirii**
- Julius Caesar – William Shakespear
- Man of Kafira – Francis Imbuga

*List of readings in Novels;*

- A man of the people – **Chinua Achebe**
- Arrows of God – Chinua Achebe
- No Longer at Ease – Chinua Achebe
- Petals of Blood – Ngugi wa Thiong'o
- A Grain of Wheat – Ngugi wa Thiong'o
- Joy Comes in the Morning – Hopolang Phororo
- The Lions of Yola – Severine Ngunguru

*List of readings in Poetry;*

- Poets of Africa 7; Boundless Voice Poem from Kenya - Arthur I. Luvai
- The Bleeding Heart and Other Poems - Shilia Kaaya.

**MICHANGO MBALIMBALI.**

**Shule za bweni;-**

**Mchango wa uendeshaji wa shule Tshs. 80,000/=**

Fedha hizi zilipwe kwenye akaunti ya shule NMB tawi lolote Tanzania bara A/C Na. 41301100021 Irkisongo Sekondari aje na slip ya benki yenye jina la mwanafunzi na si jina la mzazi.

**MUHIMU**

Nembo ya shule Tshs. 5,000/-

T-shirt ya shule Tshs. 15,000/-

**Nembo ya shule na T-shirt zinapatikana shuleni, hivyo mwanafunzi aje na fedha mkononi.**

**VIFAA VINGINE ATAKAVYOLETA**

- Godoro moja jipya la kitambaa urefu futi 6 na upana futi mbili na nusu (6 kwa $2^1/_2$)
- Shuka mbili za rangi ya **blue**
- Aje na blanketi moja zito
- Sanduku la bati lenye kufuli imara
- Aje na neti nyeupe ya kuzuia mbu
- Aje na doti moja ya kitenge cha kujifunga wakati wa kuoga tu pamoja na ndala jozi moja **(haruhusiwi kuvaa kitenge wala ndala nje ya bweni)**
- Dawa ya meno, mswaki, mafuta ya kujipaka na sabuni (**Hairuhusiwi kutumia vipodozi vya aina yoyote**).
- Ndoo ndogo mbili za lita kumi kwa ajili ya kuhifadhia maji ya kunywa na kuogea
- Tochi ya betri au taa ya kutumia mwanga wa jua. (**hairuhusiwi kutumia taa inayotumia umeme, mafuta ya taa au mshumaa)**
- Aje na **Ream (A4)** ya karatasi **mbili (2)** kwa mwaka.
- Aje na akaunti ya benki ambayo ataitumia katika kutunzia na kutoa fedha kwa ajili ya matumizi yake binafsi na pia wewe mzazi/mlezi utaitumia katika kumtumia fedha mwanao na **si vinginevyo.**

**A. VIFAA VYA USAFI**

- HGL - Fyekeo (slasher), rubber squizer na reki
- HGK - Fyekeo (slasher), dekio la tambi na rubber squizer
- EGM - Jembe (hoe), brashi laini (soft broom) na brashi ngumu (hard broom)
- HKL - Jembe (hoe), toilet brush na Brashi ngumu (hard broom) toilet brush na Brashi
- HGFa –Rubber squizer (slasher), jembe, cobweb broom (mfagio wa buibui)
- HGLi - Rubber squizer (slasher), jembe, cobweb broom (mfagio wa buibui)

**VYOMBO VYA CHAKULA.**

- Sahani ya bati (aluminium) yenye sehemu ya mboga, ugali na matunda.
- Kikombe kimoja cha bati (aluminium)
- Kijiko kimoja
- **Vyombo vya plastiki haviruhusiwi kabisa.**

**MUHIMU.**

- Kila mwanafunzi aje na cheti cha kuhitimu kidato cha nne, result slip, cheti cha kuzaliwa pamoja na nakala ya kila cheti.
- Shule haitoi chakula maalum kwa wanafunzi wenye matatizo ya kiafya kwani chakula cha shule ni kizuri.
- **Waje na bima ya NHIF au CHF. Kwa wanaotoka nje ya Mkoa wa Arusha na hawana kadi za NHIF, waje na Tshs. 6,000/= ili kukata kadi ya CHF shuleni.**
- Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani
- Mwanafunzi haruhusiwi kuja na chakula chochote shuleni.
- Mwanafunzi hatakiwi kuchelewa kuripoti kwa tarehe iliyopangwa.
- Mwanafunzi haruhusiwi kupaka rangi kucha, kupaka lipstick, aidha aje amenyoa nywele na zilingane pande zote.

**B. FOMU 1, na 2,**

**FOMU 1** ijazwe na mwanafunzi mwenyewe na mzazi au mlezi au Taasisi husika**. FOMU 2** ijazwe na daktari aliyeidhinishwa. Fomu zote 2 zirudishwe shuleni mwanafunzi anaporipoti. Shule ina zahanati inayotoa huduma ya kwanza. Aidha matibabu yanapatikana Hospitali ya Wilaya kwa gharama za mzazi au mlezi.

Tarehe ya kuripoti (Mtatangaziwa na serikali).Mwanafunzi atatakiwa afike siku za kazi zilizopangwa kabla ya saa 10:00 jioni bila kukosa .Aje na fomu zote zilizoambatishwa na barua hii zikiwa zimejazwa kikamilifu na wahusika.

**"SIMU ZA MKONONI HAZIRUHUSIWI KABISA KWA MWANAFUNZI"**

**"ELIMU NI UKOMBOZI"**
**KARIBU SANA IRKISONGO.**

HEADMISTRESS
IRKISONGO
SECONDARY SCHOOL

**NYANYAMA B. CHIREMEJI**
**MKUU WA SHULE.**

**SEHEMU HII IJAZWE NA MWANAFUNZI** F1

**MWENYEWE KWA HERUFI KUBWA**

1. (i) **JINA LA MWANAFUNZI ( Kama ilivyotumika kidato cha nne) .......................................................**

Tarehe ya kuzaliwa…………………MKOA…………….......…… WILAYA…………........................

KATA................................. KIJIJI/MTAA....................................

**2. TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI**

(i) Baba mzazi au mlezi…………………………...... Kazi yake .................. Dini........................

.Dhehebu...............................Anwani..................................Namba za Simu................................

(ii) Mama mzazi au mlezi……………….…………...... Kazi yake .................. Dini.......................

.Dhehebu...............................Anwani..................................Namba za Simu....................................

(iv) Mwanafunzi anaishi na (weka V sehemu iliyo sahihi )

(a) Baba tu { } (b) Mama tu{ } (c) Wazazi wote wawili { }(d) Mlezi { } (e) shirikani { } (f) kituo cha malezi { }

**3. MZAZI/MLEZI/ TAASISI ITAYOGHARAMIA MAHITAJI YA SHULE:**

(i) Jina …………………………………………………………………………………………………….

(ii) Kazi yake ni …………………………………………………………………………………………….

(iii)Anuani ya mzazi/Mlezi ……………………………………………………………………………

(iv) Namba yake ya simu…………………………………………………………………………………

(v) Uhusiano wake………………………………………………………..Mf. Baba, Mama, Dada, Mjomba au mfadhili.

**4. UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI**:

Mimi ……………………………………...... nakubali kujiunga na shule ya **SEKONDARI IRKISONGO** na kuthibitisha kuwa, nitafuata sheria na taratibu zote za shule hii ili nitimize lengo la kuja shuleni kwa

manufaa yangu binafsi, familia na Taifa kwa ujumla. Endapo nitakwenda kinyume na sheria/kanuni/taratibu za shule nitakubali kuadhibiwa.

**Sahihi ya mwanafunzi ………………………………………………….tarehe……………………...................**

F1

**5. NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI**

Mimi Mzazi/Mlezi nathibitisha kuwa waliojiandikisha hapo chini ni ndugu zangu wa karibu ambao wanaweza kushirikishwa mwenendo wa mwanafunzi pindi itakapohitajika.

| S/N | MAJINA MATATU | UHUSIANO NA MTOTO | PICHA YAKE (PASSPORT SIZE) | SIMU YA MKONONI | SAINI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | |
| 2. | | | | | |
| 3. | | | | | |
| 4. | | | | | |

**NB: Hataruhusiwa mtu ambaye si mhusika na hajaorodheshwa kwenye fomu kuja kwa masuala yeyote yanayomhusu mwanafunzi shuleni.**

F2

**PRIME MINISTER'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**IRKISONGO SECONDARY SCHOOL**

**MEDICAL EXAMINATION**

To THE MEDICAL OFFICER (GOVERNMENT HOSPITAL)
..................................................................
....................................................

Please examine the above named student and arrange for any necessary treatment for a student if need.

HEADMISTRESS
IRKISONGO
SECONDARY SCHOOL

**THE HEADMISTRESS.**

Student's full name: …………………………………… Age:-…………Year.................

REMARKS

SKIN.......................................................................................................................................
EYES......................................................................................................................................
EARS......................................................................................................................................
TEETH....................................................................................................................................
B/S TEST (CHRONIC)..........................................................................................................
PRESURE..............................................................................................................................
ABDOMEN............................................................................................................................
CHEST...................................................................................................................................
STOMACH.............................................................................................................................
URINE...................................................................................................................................
HB.HAEMOGLOBIN..........................................................................................................
T.B TEST:-………………………………………………………………...........................................
VDRL.....................................................................................................................................
HIV TEST: ............................................................................................................................
UPT TEST.............................................................................................................................
STOOL...................................................................................................................................
ULCERS...............................................................................................................................
DIABETIC.............................................................................................................................
ASTHMATIC.........................................................................................................................

Doctors Name.......................................... Signature: ………………………………
Designation ………………………………..................... Station ………………………………

## SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE KWA WANAFUNZI

### 1. Sheria na kanuni muhimu za shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria, Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamira ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo yanayofafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 1.1 Sheria na kanuni za shule

**(a)** Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

**(b)** Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.

**(c)** Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku (Preparation)

**(d)** Kuwahi katika kila shughuli za Shule utakazopewa

**(e)** Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika Shule hii.

**(f)** Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya Shule

**(g)** Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

**(h)** Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

**(i)** Kutunza mali za shule

**(j)** Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari na;

**(k)** Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kushawishiwa na mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

## MUHIMU;

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.

- ❖ Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.
- ❖ Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa shule. (Msiba au Ugonjwa)

**1.2 Makosa yatakayosababisha mwanafunzi kufukuzwa shule ni pamoja na;**

a. Wizi
b. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
c. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
d. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
e. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
f. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
g. Kufuga ndevu.
h. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya.
i. Uvutaji wa sigara.
j. Uasherati, mahusiano ya jinsia moja, kuoa au kuolewa.
k. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
l. Kusababisha mimba.
m. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
n. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.
o. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
p. Kudharau bendera ya Taifa.
q. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu na;
r. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi

**2. Viambatisho na Fomu muhimu.**

i. Fomu ya uchunguzi wa Afya (Medical Edamination Form) ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa Hospitali ya serikali.
ii. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule. na;
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

**3. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa shule**

**Jina la Mkuu wa shule: <u>NYANYAMA BWIRE CHIREMEJI</u>**

**Mhuri wa Mkuu wa shule** HEADMISTRESS IRKISONGO SECONDARY SCHOOL

**NB:** Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.

***TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO;***

- **Mkuu wa shule: 0752 954 965**
- **Makamu mkuu wa shule: 0621 291 852**
- **Mwandamizi Taaluma: 0763 874 825/0716 772 876**
- **Mwandamizi malezi: 0758 463 574**